# HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE

**SHULE YA SEKONDARI SUMA,**

**S.L.P 341,**

**TUKUYU.**

**SIMU *0754917191* (MKUU WA SHULE), *0762595756*(MAKAMU MKUU)**

**MZAZI/MLEZI WA______________________________________________**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI SUMA MWAKA 2021**

Ninafuraha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari Suma kidato cha **KWANZA** mwaka 2021. Shule ipo umbali wa km13 kaskazini Mashariki mwa mji wa Tukuyu. Usafiri wa basi unapatikana katika kituo cha mabasi Katumba barabara ya Mwakaleli.
Muhula wa masomo utaanza tarehe 11.01.2020 hivyo unatikiwa kuripoti shuleni mapema iwezekanavyo.

**MAMBO YA KUZINGATIA**.
**1.SARE ZA SHULE**. 1. Suruali/sketirangi ya kijani na damu ya mzee kwa wavulana na wasichana sketi ndefu. 2. Mashati mawili ya mikono mifupi (tomato), hijabu ya rangi nyeupe kwa waislam.
3. Viatu vyeusi vya kamba pea mbili vyenye kisigino kifupi na kiwi nyeusi.
4. Masweta mawili damu ya mzee na kijani.
5. Tai mbili rangi ya damu ya mzee na kijani.
6. Soksi pea mbili nyeupe kwa wasichana na nyeusi kwa wavulana.
7. Wavulana waje na mkanada mweusi usio na chata yoyote.
8. Sare ya michezo ni T-shirt na bukta au traki suti rangi ya zambarau (**Mbeya city**) kwa wavulana na wasichana,na raba.
9. Fagio/chelewa kwa ajili ya usafi eneo utakalopangiwa kufanya usafi.
10. Ndoo moja ya lita 10 kwa ajili ya kuhifadhi maji.

**2. VIFAA VINGINE.**
1. Daftari kubwa (**counter book)** 12, mkebe wa hisabati na peni.

**3. MAHITAJI YA CHAKULA.**
Mahitaji ya chakula kwa wanafunzi wa kutwa ni wajibu wa mzazi/mlezi kuhakikisha anachangia chakula kama itakavyoelekezwa na kamati ya chakula katika kikao cha wazazi.

**4.MCHANGANUO WA GHARAMA ZA BWENI (HOSTEL) KWA WASICHANA**. Kwa wanafunzi wa bweni/hostel gharama zake ni kama ifuatavyo;

**1. GHARAMA ZA CHAKULA KWA MWANAFUNZI MMOJA KWA MWAKA NI TSH.366,000/=**

| S/N | AINA YA CHAKULA | KIPIMO | KIASI |
|---|---|---|---|
| 1 | MAHINDI YALIYOKOBOLEWA | DEBE 7 | 110,000/= |
| 2 | MAHARAGE | DEBE 3 | 90,000/= |
| 3 | MCHELE | DEBE 2 | 80,000/= |
| 4 | NYAMA | KILO 8 | 40,000/= |
| 5 | MAFUTA YA KULA | LITA 8 | 32,000/= |
| 6 | VIUNGO (CHUMVI,NYANYA NAVITUNGUU) | | 12,000/= |
| 7 | KUNI | | 20,000/= |
| 8 | MBOGAMBOGA | | 10,000/= |
| | | **JUMLA** | **394,000/=** |

**ANGALIZO. Hakuna chakula maalum (SPECIAL DIET)**

**2. MICHANGO MINGINE.**

| S/N | AINA YA MCHANGO | KIASI |
|---|---|---|
| 1 | MATRON | 20,000/= |
| 2 | MPISHI | 20,000/= |
| 3 | MATIBABU | 10,000/= |
| 4 | UKARABATI | 10,000/= |
| | **JUMLA** | **60,000/=** |

Jumla ya gharama za uendeshaji wa bweni/hostel ni **Tsh. 454,000/=** kwa mwaka. Gharama hizi zinajumuisha **chakula** na **michango mingine** kama ilivyoainishwa kwenye majedwali hapo juu.

**AWAMU ZA MALIPO**

| **MALIPO** | **AWAMU 1** | **AWAMU 2** | **AWAMU 3** | **AWAMU 4** | **JUMLA** |
|---|---|---|---|---|---|
| **KIASI** | **150,000/=** | **110,000/=** | **100,000/=** | **94,000/=** | **454,000/=** |

**VIFAA VINGINE KWA WANAFUNZI WA BWENI.**

1. Nguo za kushindia baada ya masomo(shamba dress) ni gauni 2 za rangi ya kijani.
2. Mashuka 2 ya rangi ya pink na blue, mto na folonya.
3. Blanketi 1 zito rangi yoyote.
4. Chandarua kimoja rangi ya blue.
5. Godoro 1 futi mbili na nusu kwa sita($2^{1/2}$x6).
6. Sahani 1 ya alluminium/bati, bakuli, kikombe na kijiko.
7. Tranka la chuma/mbao
8. Ndoo mbili za lita kumi kwa ajili ya usafi na kuhifadhi maji.
9. Vifaa vya usafi(jembe,fyekeo,fagio na mopa).

10. Sabuni ya kufulia na kuogea, mswaki,dawa, mafuta ya kupaka taulo na toilet paper 3.
11. Kila mwanafunzi atajitegemea sukari kwa kila muhula.
12. Ndala za kuogea, nguo za ndani za kutoshana na sweta la kujikinga na baridi.

**6.SHERIA NA KANUNI ZA SHULE**

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa ***Sheaia ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978***. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini.Hivyo utatakiwa kuzingatia mambo ya msingi kama ifuatavyo(a)Heshima kwa Viongozi, Wazazi, Wafanyakazi wote, Wanafunzi wote wengine na jamii kwa ujumla.

(b)Kuwa na mahudhulio mazuri siku zote shuleni (Darasani na kazi za nje)

(c) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (Preparation).

(d) Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopewa.

(e) Kifahamu mipaka ya shule na kuwepo ndani ya shule na kutoka nje kwa kibali cha shule.

(f) Kutunza mali ya shule usafi wa mwili na mazingira ya shule.

(g) Kuvaa sale za shule wakati wote unapotakiwa.

(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

(i) Kuheshimu Bendera ya Taifa ,Wimbo wa Taifa na wa shule.

**7.MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA UKAFUKUZWA SHULE**

(a)Wizi (b)Uasherati,Ubakaji na Ushoga (c) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya (d)Uvutaji bangi (e)Makosa ya jinai (f)Kupiga au kupigana(g)Kuharibu kwa makusudi mali ya shule (h)Kudharau Bendera ya Taifa(i)Kuoa au kuolewa (j)Kupata mimba ndani na nje ya shule(k)Kukataa adhabu kwa makusudi(l)Kugoma,kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu(m)Kuwa na simu shuleni

**8.MAMBO MENGINE MUHIMU.**

(i)Medical Examination Form ambayo itajazwa Mganga mkuu wa Hospitali ya Serikali fomu hii itakabidhiwa shuleni utakapo ripoti.

(ii)Fomu ya mkataba na shule iliyojazwa na mwanafunzi na mzazi/mlezi

***N:B.Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo na kuyatekeleza yote.***

**‘ KWA PAMOJA TUJENGE SUMA YETU KARIBU SANA’**

______________________________

SADICK Z CHAULA

**MKUU WA SHULE**